## Kwa maelekezo ya ziada:

Wanawake na wanaume wote wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka milima ya Tao la Mashariki wanahaki ya kuhusishwa katika shughuli za uhifadhi wa mazingira na misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Wanaweza kupata maelekezo ya ziada kutoka kwa viongozi wao wa vijiji, kata na wabunge.

## Mabadiliko ya Tabianchi

Badiliko linalopimwa katika hali ya hewa linalodumu kwa kipindi kirefu (hasa miongo) na husababishwa zaidi na shughuli za kibinadamu. Madhara yake: uzalishaji duni, magonjwa, upotevu wa mali na maisha, kuongezeka kwa gesijoto na uhamisho. Ushahidi: Kuyeyuka kwa barafu ya milima mirefu kama Kilimanjaro, mafuriko, kuongezeka kwa joto, ukame na uchafuzi wa hewa.



**MKUHUMI:** Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutokana na ufyekaji na Uharibifu wa Misitu. Faida zake: kupunguza uzalishaji wa gesi joto; kutunza bioanuwai na katika masuala ya usimamizi wa ikolojia; kuongeza kipato kwa jamii; na kuchangia katika gharama za usimamizi wa misitu.


## Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Ni shirika lisilo la kiserikali lililoanzishwa 1985 lenye lengo la kuhifadhi na kurejesha misitu yenye bioanuwai muhimu kitaifa na kimataifa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Linafanya kazi na jamii na wadau wanaoizunguka misitu ya milima ya Tao la Mashariki na Ukanda wa Pwani.

## Hazina ya Mazingira yaliyo katika hali ya Kuangamizwa (CEPF)

CEPF inafadhili uhifadhi wa maeneo nyeti ya bioanuwai duniani na ambayo yako katika hali ya kuangamizwa kutokana na uharibifu wa mazingira. Hapa Tanzania ni misitu ya Milima ya Tao la Mashariki na Ukanda wa Pwani. CEPF ni juhudi za pamoja zilizojumuisha shirika la Conservation International, Mfuko wa kimataifa wa kuhifadhi mazingira (GEF), serikali ya Japan, taasisi ya maendeleo ya Ufaransa, taasisi ya MacAthur na Benki ya Dunia.


Kwa mawasiliano:
Mkurugenzi Mtendaji,
Tanzania Forest Conservation Group
(Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili
Tanzania): TFCG
S.L.P. 23410, Dar es Salaam
Simu:+255 22 2669007
Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz
Tovuti: www.tfcg.org

# Jamii na Uhifadhi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania



## Misitu ya  Milima ya Tao la Mashariki

Milima ya Tao la Mashariki ni safu ya milima ya kale, inayoaminika kuwapo zaidi ya miaka milioni 30, yenye misitu iliyosambaa kuanzia Kenya hadi Tanzania.

## Inapatikana wapi?

Kuna safu ya milima 12 inayotengeneza Milima ya Tao la Mashariki kwa upande wa Tanzania, na imepita katika wilaya za Mwanga, Same, Lushoto, Korogwe, Muheza, Mkinga, Kilindi, Morogoro, Mvomero, Kilosa, Ulanga, Kilombero, Kilolo, Mufindi na Mpwapwa.

## Bioanuwai

Misitu ya milima hii ina bioanuwai nyingi na za kipekee. Kuna aina za kipekee za mimea 500, mamalia 10, ndege 19, repitilia 29 na jamii ya vyura 100. Bioanuwai nyingi zipo hatarini au katika tishio kwenye eneo hili nyeti.

## Maji

Kilimo, viwanda na matumizi ya nyumbani yanategemea maji kutoka Milima ya Tao la Mashariki. Eneo hili nyeti ni chanzo cha mito mingi ikiwemo Ruvu, Sigi, Wami, Ruaha na Pangani. Maji yake huzalisha zaidi ya asilimia 60 ya umeme wa Tanzania.

## Udongo

Misitu husaidia kuhifadhi udongo. Misitu ya Tao la Mashariki huzuia mmomonyoko na maporomoko ya ardhi.



## Nini jamii ifanye ili kuinusuru misitu ya milima ya Tao la Mashariki?

Zaidi ya 70% ya misitu ya asili ya Milima hii imeharibiwa. Jamii inatakiwa iwe na welewa ili, iweze kuondoa matatizo yaliyoko ambayo ni moto, uvunaji wa mbao na kuni usio endelevu, uchimbaji wa madini, na uwindaji haramu.

## Jamii ifanye nini ili kuhifadhi misitu ya Milima ya Tao la Mashariki na kuboresha maisha yao?

Jamii inaweza; kupanda miti, kufuga nyuki, kufuga samaki, kushiriki katika ulinzi wa msitu, kushiriki katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu, na kuendeleza kilimo endelevu.

## Usimamizi wa Misitu ya Jamii (UMJ)

Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) ni pamoja na Usimamizi wa Misitu ya Jamii (UMJ) na Usimamizi wa Pamoja wa Misitu (UPM). Kutokana na uharibifu wa misitu kuna mabadiliko ya kisheria na sera za misitu.  Mabadiliko haya yametoa fursa kwa wananchi kusimamia misitu kwa njia endelevu ambapo majukumu ya kusimamia yamewekwa katika ngazi ya jamii/kijiji, kikundi au watu binafsi. Fursa hii inawapa jamii wajibu wa kuanzisha/ kuunda misitu ya hifadhi ya vijiji.





## Mpango wa matumizi bora ya ardhi

Mpango / mwongozo unaowawezesha wanakijiji kufanya maamuzi ya ardhi yao kwa kuzingatia utaalamu. Mpango huu unapunguza na kutatua migogoro ya ardhi inayotokana na matumizi ya ardhi. Wananchi wanapata fursa ya kutenga maeneo na kutungia sheria ndogo ambazo zinasimamiwa na halmashauri ya kijiji.

## Upandaji miti

Jamii na shule zinaweza kupanda miti kwa kuanza na kuandaa na kuendeleza vitalu vya miti. Ni vema kila kaya, taasisi na jamii ikapanda miti katika eneo lao ili tuokoe sayari yetu na uharibifu wa mazingira, na vilevile tupate maendeleo endelevu. Ni vema tupande miti inayostawi katika eneo letu na hasa miti ya asili.

## Ufugaji Nyuki

Ufugaji wa nyuki unasaidia kuhifadhi mazingira. Ufugaji nyuki unahitaji mimea ikiwemo miti. Faida za ufugaji nyuki: kuhifadhi mazingira, asali ni chakula, kuongeza kipato. Nta ambayo hutumika viwandani kutengeneza bidhaa anuwai.

